JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

**BARAZA LA FAMASI**

# UHUISHAJI WA TAARIFA ZA WANATAALUMA KWA MWAKA 2026

## UTANGULIZI

1. **DHUMUNI**: Kutekeleza takwa la Vifungu Na. 22, 26 na 30 vya Sheria ya Famasi, Sura 311 (The Pharmacy Act, Cap 311).
2. **WAHUSIKA**: Wafamasia, Fundi Dawa Sanifu na Fundi Dawa Wasaidizi.
3. **MFUMO WA UHUISHAJI**: Mfumo wa Kielektroniki unamtaka mwanataaluma kuwasilisha taarifa zake za sasa katika Ofisi ya Msajili kwa mujibu wa Sheria na kuchapisha (printing) leseni ya utendaji kupitia mfumo wa kielektroniki.

## UTARATIBU WA KUHUISHA TAARIFA ZA MWANATAALUMA KWENYE REJESTA

**a**) **FOMU**: Jaza fomu inayopatikana kwenye tovuti www.pc.go.tz kisha bonyeza huduma za kimtandao (Online Services Menu) kisha bonyeza Retention Application;

- *Sign up*: Kwa mwanataaluma ambaye hajawahi kujisajili: *Pharmacist Sign Up*.
- Kwa mwenye akaunti: tumia nywila ya awali kupitia PCMIS.

**b**) **ADA:** Utapaswa kulipa ada ya kuhuisha usajili kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Wanataaluma ya mwaka 2005 na Kanuni za Ada na Tozo ya mwaka 2012 kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Mfamasia | TZS 165,000/- |
| Fundi dawa sanifu | TZS 66,000/- |
| Fundi dawa msaidizi | TZS 44,000/- |

**b**) **MUDA WA MALIPO**: Dirisha la maombi litafunguliwa tarehe **08/12/2025** na mwisho wa kulipia ada ni tarehe **31/01/2026**, baada ya hapo utalazimika kulipa faini ya asilimia ishirini na tano (25%) ya kiwango ulichotakiwa kulipia.

## MAMBO YA KUZINGATIWA WAKATI WA KUHUISHA TAARIFA ZAKO KWENYE REJESTA

**a**) **JINA**: Kama lilivyoainishwa katika cheti cha usajli kilichotolewa na Baraza (Registration, Enrollment, or Enlisting Certificate);

**b**) **NAMBA YA USAJILI**: (Registration, Enrollment or Enlisting Number): Personal Identification Number (PIN) mfano: -

| S/N | KADA | NAMBA YA USAJILI | KEY CODE | PIN (PERSONAL IDENTIFICATION NUMBER) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfamasia | 754 | 01 | 0000000 mfano 0100754 |
| 2. | Fundi Dawa Sanifu | 1010 | 04 | 0000000 mfano 0401010 |
| 3. | Fundi Dawa Msaidizi | 24 | 05 | 0000000 mfano 0500024 |

**c**) **PICHA** (**Kwa mwanataaluma ambaye hajaweka picha):**
Nakala laini ya picha (upload passport size photo) yenye Background ya bluu. Zingatia vipimo upana *350px* urefu *350px* kama mfano ufuatao;





**d**) **MAFUNZO ENDELEVU**

(*Continuing Professional Development – CPD, Additional Qualification*-Mf. *Masters, PHD, Professor, Other continuing Education - CE*): Wasilisha nakala laini ya vyeti vya mafunzo endelevu vya aidha kozi za muda mrefu au muda mfupi;

**e**) **LESENI YA UTENDAJI KAZI**:

I. Leseni za utendaji kwa sasa zinatolewa kwa njia ya mfumo wa kielektroniki wa Baraza (PCMIS) kupitia akaunti za Wanataaluma.

II. Baada ya kukamilisha maombi ya kuhuisha taarifa kwenye rejesta, Mwanataaluma ataweza kuchapisha (printing) leseni yake ya utendaji wa taaluma kupitia mfumo wa PCMIS.

**f) MALIPO:**

- Ankara ya malipo (*Control number*) itapatikana kwenye mfumo (*automatically*) wakati wa kuwasilishwa maombi sehemu ya Bill Creation na kutumwa kwenye namba yako ya simu.
- Ankara ya malipo itaisha muda wake tarehe **31/01/2026**.
- Utatakiwa kutembelea akaunti yako sehemu ya *Bill Creation* kuweza kupata ankara mpya ya malipo endapo utafanya malipo baada ya tarehe **31/01/2026** ambayo itaambatana na faini ya 25%: